# Kauli za Utendwa/utendewa katika Tamthilia za *Machozi ya Mwanamke* na *Heshima Yangu*

E. Mahenge


## Ikisiri

Kazi hii ni ya utafiti wa kiisimu mitindo unaolenga kulinganisha na kulinganua kazi mbili za tamthiliya za Kiswahili ambazo ni *Heshima Yangu* (Muhando, 1974) na *Machozi ya Mwanamke* (Ngozi, 1977). Kwanza, makala inachunguza matumizi ya kauli za utendwa/utendewa katika tamthiliya hizi ili kujua kama ni ya hiari au shinikizo la muktadha. Vilevile lengo ni kujua tofauti ya matumizi hayo kwa waandishi hawa ili kuona wana mwelekeo gani. Pili, makala inatafuta sababu za matumizi haya ya kauli zenye utendwa/utendewa katika tamthiliya hizo. Baada ya hapo, makala inachunguza aina za utendwa/utendewa zilizojitokeza katika tamthiliya hizo. Dai tete linaloongoza makala hii ni kwamba, katika tamthilia hizi mbili, wanaume wanatumia kwa wingi kauli zenye utendwa kuliko wanawake.


## 1.0 Utangulizi

Katika schemu hii tutajadili suala linalodadisiwa kuhusu matumizi ya kauli ya utendwa kama ni suala la uchaguzi wa hiari au ni shinikizo la kimuktadha. Fikra ya msingi katika suala zima la mtindo ni uchaguzi, kwa hiyo mahali ambapo hapana uchaguzi basi hapo hapana mtindo. Kwa maneno mengine uchaguzi huu ni wa kutumia kauli za utendwa/utendewa badala ya kauli za utenda.

Katika kazi hii si kila utumiaji wa kauli ya utendwa ni uchaguzi wa hiari wa msemaji bali kuna wakati kunakuwepo na ulazima wa kutumia kauli hizo. Ulazima huu ni *shinikizo la kimuktadha*, nao hutokana na asili ya kitenzi. Mathalani, kama kitenzi mahsusi kinahusisha mahusiano ya ngono, hakuna namna inayowezesha mwanamke kama ndiye kiima cha sentensi kusema mawazo yake katika kauli ya utenda. Hapa ndipo ulazima au shinikizo la muktadha linapojitokeza.

Kwa upande mwingine kuna suala la *uhiari* katika matumizi ama ya kauli ya utendwa, utendewa au utenda. Jambo hili la kuzungumza mawazo yaleyale katika kauli ya utendwa/utendewa na utenda hutokana na aina ya vitenzi husika. Iwapo vitenzi hivyo havihusiani na masuala ya mahusiano ya ngono, upo uwezekano wa kufanya uchaguzi wa hiari. Tunaweza kusema kuwa suala la uchaguzi linatokana na sababu mbalimbali zinazompa uhuru msemaji ili aweze kuchagua namna ya kusema wazo lake katika kauli ya utendwa/utendewa au kauli ya utenda.

Vilevile katika lugha ya Kiswahili yapo matendo ambayo yana umbo linaloonekana kama ni la utendwa/utendewa lakini hayamaanishi utendwa/utendewa bali ni muundo wenyewe wa vitenzi hivyo ndivyo ulivyo. Matendo haya huelezea uzoefu hasi, hasa wenye kuhusiana na matatizo, kama vile ukisema **"ninaumwa"** na **"nimefiwa"**. Matendo haya hayamaanishi kutendewa jambo hilo, bali ndivyo lugha inavyotumika.

Kwa upande mwingine, katika Kiswahili kuna utamaduni ambao umejificha na hujieleza kupitia lugha yenyewe. Mathalani, kuna matendo yanayohusisha mahusiano ya kingono kuwa katika pande mbili yaani yapo katika hali ya utenda na katika hali ya utendwa/utendewa. Kwa kawaida wanaume wengi hawako huru kuelezea mahusiano haya katika utendewa/utendwa yaani kusema: **"nimeolewa"**,**"nimeposwa"**, **"nimechumbiwa"**, **"nimetolewa mahari"** na **"nimetongozwa"** kama ilivyo kwa wanawake. Wengi wa wanaume hawa hulazimishwa na utamaduni wa lugha ya Kiswahili kutumia kauli ya utendaji tu, yaani kusema:- **"nimeoa"**, **"nimeposa"**, **"nimechumbia"**, **"nimetoa mahari"** na **"nimetongoza"**.

Na kwa upande wa wanawake wengi wao hutumia kauli ya utendwa/utendewa katika kuelezea mahusiano ya kingono u ya kimapenzi kama vile: **"nimeolewa"**, **"nimetolewa posa"**, **"nimechumbiwa"**, **"nimetongozwa"** na **"nimeposwa"**. Ni katika jamii chache tu, kwa mfano, kwa wakurya, ambapo baadhi ya wanawake hutumia kauli ya utenda katika kuelezea mahusiano haya kama vile: **"nimeoa"**, **"nimeposa"**, **"nimechumbia"**, **"nimetoa mahari"** na **"nimetongoza"** kufuatana na utamaduni wao wa mwanamke kuweza "kumwoa" mwanamke mwenziwe. Na vilevile si kwa wanaume wote wana uhuru wa kutumia kauli za utendewa/utendwa isipokuwa wale ambao ni mashoga.

Kwa maana hiyo makala hii inapingana na kauli ya Lakoff (1975) inayodai kuwa wanawake hunyanyaswa mara mbili: kwanza kwa jinsi lugha inavyotumika kuwazungumzia wao, na pili jinsi wanavyokuzwa na kufundishwa namna ya kutumia lugha. Jambo hili si kila mahali kwani tumeona wazi jinsi wanawake na wanaume katika utamaduni wa lugha ya Kiswahili wanavyoweza kutumia kauli zote mbili, yaani kauli ya utenda na kauli ya utendwa/utendewa katika kuelezea mahusiano ya kingono.

Historia ya jambo hili inaonesha kuwa kazi nyingi na tafiti nyingi zilizohusisha kauli hii ya utendwa/utendewa katika lugha ya Kiswahili zimeshughulikiwa kwa namna mbili, yaani: **kidhima** na **kikategoria**. Kidhima kauli ya utendewa/utendwa ina kiima na chagizo wakati kikategoria kauli ya utendewa/utendwa ina kirai nomino (KN) na kirai kihusishi (Kh). Kwa upande mwingine, kauli ya utenda inaweza kufafanuliwa kwa namna mbili, yaani: kidhima na kikategoria. Kidhima kauli ya utenda ina kiima (katika kiima kuna nomino) na kiarifu (katika kiarifu kuna kitenzi na yambwa). Na kikategoria kauli ya utenda ina kirai nomino (ambacho kinakaliwa na nomino) na kuna kirai kitenzi (ambacho kinakaliwa na kitenzi na nomino).

Mbali na kauli ya utendwa/utendewa kuwa na matumizi makubwa katika uwanja wa lugha ya Kiswahili, hakuna utafiti ambao umeshafanywa kuhusu kipengele hiki cha kauli ya utendwa/utendewa kama mbinu ya kiisimu mitindo. Mkude (2005) ndiye pekee aliyechambua vichwa vya habari vyenye kauli za utendwa katika magazeti ya *Nipashe*. Ukiachilia mbali kazi hiyo, hakuna mhakiki mwingine katika lugha ya Kiswahili aliyechunguza kipengele hiki isipokuwa wale waliotoa fasili ya kauli ya utendwa/utendewa kidhima au kikategoria. Na katika kazi ya hiyo Mkude, mwandishi alionesha wazi kuwa kauli ya utendwa ni kitu muhimu sana katika uchambuzi wa mazungumzo hasa katika muktadha wa Kiafrika; ikizingatiwa kuwa watoto wa Kiafrika huweza kutumia kauli za utendwa/utendewa mapema zaidi ikilinganishwa na wenzao wa jamii za Kizungu.

Makala hii imelenga kuleta pamoja mkabala wa kiisimu (kwa kutumia kipengele cha kauli ya utendwa/utendewa) na ule wa kifasihi (kwa kutumia nadharia ya uchambuzi wa kifasihi) kwa lengo la kuchunguza ni kwa jinsi gani matumizi ya lugha yanaweza kuathiri mawazo ya mwandishi au mzungumzaji wa lugha. Suala hili limefanyika kwa kuchukua kipengele kimoja cha kiisimu kijulikanacho kama utendwa/utendewa katika tamthiliya za *Machozi ya Mwanamke* (Ngozi, 1977) na *Heshima Yangu* (Muhando,1974). Uchambuzi wa nyaraka ambao ulikuwa ni wa kisarufi umewezesha kukamilisha lengo la makala hii ambalo ni kujua sababu za matumizi ya kauli za utendwa/utendewa na kujua kama matumizi hayo ni ya hiari wakati wote na katika mazingira yote. Makala inazipambanisha tamthilia hizo mbili ili kuona kama kuna tofauti yoyote baina ya tamthilia hizo kufuatana na masuala yaliyoshughulikiwa na kila mwandishi.

Makala hii imekusudia kuongeza uelewa wa kipengele hiki cha kauli ya utendwa/ utendewa. Pia inatarajiwa kuwa itatoa mchango katika uchambuzi wa kazi za kifasihi na zisizo za kifasihi kwa kutumia kipengele cha kisintaksia kama mbinu ya kiisimu mitindo. Vilevile inatarajiwa kuwa makala hii itatoa mchango katika uwanja wa kazi za kiuchambuzi za Kiswahili kwa sababu bado hakuna mhakiki aliyetumia kipengele hiki cha kisintaksia kama mbinu ya kimitindo. Kwa njia hii, inatarajiwa kuwa makala itaongeza uelewa wa dhana ya mtindo kwa kutumia kauli ya utendwa/utendewa kama kipengele cha uchambuzi wa kazi za kifasihi na kama kipengele cha kimitindo.

Nadharia inayoongoza uchambuzi huu ni ile ya mtindo kama ilivyojadiliwa na Crystal (1969), Enkenvist (1973) na Leech na Short (1981). Mtindo unachukuliwa kuwa ni utofauti uliopo baina ya mwandishi mmoja na mwingine. Na kwa upande mwingine, mtindo unachukuliwa kuwa ni uchaguzi anaoufanya mwandishi, wa kutumia kipengele "x" badala ya kipengele ":y" katika kazi yake. Katika uchambuzi wetu wa tamthiliya hizi mbili tumetumia fasili ya mtindo kama uchaguzi wa mwandishi; yaani uchaguzi anaoweza kuufanya mwandishi kati ya ama matumizi ya kauli ya utendwa/utendewa au utenda.

## 2.0 Uchambuzi wa kimitindo

Uchambuzi wa kimitindo unafuata hatua kadhaa. Kwanza unahusisha kuelewa maana ya matini zitakazochambuliwa. Pili, huviainisha vipengele ambavyo vitachambuliwa kwa kuviwekea vigezo vya uainishaji wake. Katika makala hii, vipengele vitakavyochambuliwa ni matumizi ya kauli zenye utendwa/utendewa katika tamthiliya hizo.Vigezo hivyo ni suala la uchaguzi: iwapo uchaguzi huo ni wa hiari au shinikizo la muktadha la kutumia kauli zenye utendwa/utendewa katika tamthilia hizi mbili.

Katika hatua ya tatu vipengele hivyo vinabainishwa au kuwekwa katika makundi mbali mbali ili kuweza kuvishughulikia kwa umakini mkubwa. Lengo la kufanya hivi ni kutaka kupata uikisadi kwa ajili ya kumbukumbu na kurahisisha uchambuzi wake ambao utaziweka kauli za utendwa/utendewa katika makundi mbalimbali ya sababu za matumizi yake ili kurahisisha zoezi hili. Baada ya hatua hizo tatu, ya nne ni ya uchambuzi wenyewe ambao unahusisha uwasilishaji wa data ambao hatimaye unahusisha tafsiri ya matokeo ya uchambuzi wetu.

## 2.1 Uchambuzi wa Data

Mkude (2005) anawasilisha sababu mbalimbali za matumizi ya kauli ya utendwa/ utendewa katika lugha ya Kiswahili zikiwemo za kudondosha nafasi ya mtenda kutokana na sababu mbalimbali kama vile kufahamika kwa mtenda kutokana na mazingira ya sentensi, egemeo la kisintaksia, kuzingatia itifaki, umuhimu wa mada, na mbinu ya kuondoa utata.

Kuchambua matumizi ya utendwa/utendewa kunahusisha michakato miwili ambayo inahusisha kubainisha vipengele tunavyovishughulikia katika uchambuzi wetu ambavyo ni matumizi ya kauli za utendwa/utendewa katika tamthiliya hizo mbili. Ubainishaji huu ulifanyika kwa kuzipa namba sentensi zote zilizoandikwa kwenye kila tamthiliya. Mchakato wa pili ni wa kubainisha vishazi vyote vyenye hali ya utendwa/utendewa.

Katika makala hii tumetumia michakato hiyo kupima matumizi ya kauli zenye utendwa/utendewa ili kubaini kama ni za hiari au za shinikizo la muktadha. Upimaji wa suala hili la uhiari na ulazima ulifanywa kwa kuzibadilisha sentensi zote zenye kauli ya utendwa/utendewa ili ziwe katika kauli ya utenda. Kilichojitokeza katika zoezi hili ni kwamba, vile vishazi vyote vyenye mfungamano na maswala ya ngono havitoi uhuru kwa kiima cha jinsia ya kike kutumia kauli ya utenda. Vilevile misemo katika lugha hii haipendezi kuwa katika kauli ya utenda. Kwa hiyo, kuna ulazima ibaki katika kauli ya utendwa/utendewa. Jambo hili linadhihirisha kuwa si kila kauli ya utendwa/utendewa ni athari ya kufanyiwa tukio fulani, lahasha. Wakati mwingine, kauli ya utendwa/utendewa ndiyo inayopendeza katika misemo na kuna ulaini fulani wa kutumia kauli hii. Unapotumia kauli ya utenda katika msemo kunakuwa na

ukakasi wa maana pamoja na ukakasi wa mazungumzo kwa kuwa hayasikiki vizuri kwa wasikilizaji au wasomaji wa kazi hiyo.

Jambo lililofuatia katika mchakato huu wa pili ni kuyagawa matumizi haya ya utendwa katika sababu mbalimbali kama vile kujulikana kwa mtenda, umuhimu wa mada, kukwepa lawama, kutojihusisha na mamlaka ya kimaamuzi na mbinu ya kuondoa utata. Vigezo vilivyotumika katika kufanya mgawo huu ni kuchunguza kishazi husika jinsi kilivyotumika katika muktadha huo na kuona kama kinahitaji kumtaja mtenda wa jambo au la.

Vipengele vya muktadha na mantiki ni muhimu sana katika mgawo huu kwani vimewezesha kuvipima vishazi na kuviweka katika sababu za matumizi ya utendwa/utendewa. Tutatoa ufafanuzi wa sababu hizi za matumizi ya utendwa/ utendewa ili kuweka bayana jambo hili. Sababu ya kwanza, ya kukwepa lawama inahusisha kutokujifungamanisha na taarifa inayotolewa kuhusu jambo fulani ili litakapogundulika mtu asihusishwe kwa namna yoyote ile. Sababu ya pili ni kutojihusisha na maamuzi ya kimamlaka, nayo hii inamwondoa mzungumzaji ili asijifunge wala kujibainisha kwa kuhusika katika kufanya maamuzi fulani ya kimamlaka. Sababu ya tatu ni kudondosha nafasi ya mtenda, jambo linalotokana na kufahamika kwa mtenda wa jambo husika. Kwa hiyo, inaonekana si muhimu kumjua wala kumtaja. Sababu ya nne ni umuhimu wa mada ya mazungumzo pale ambapo mada ni muhimu zaidi kuliko mhusika anayetajwa katika mada hiyo. Na mwisho ni sababu ya mbinu ya kuondoa utata ambapo kuna wakati kauli ya utenda ikitumika inasababisha mkanganyiko. Hivyo kwa kutumia kauli ya utendwa/utendwa husaidia kuondoa mkanganyiko au utata huo. Haya yote yametuwezesha kufanya mgawo wa vishazi vyenye utendwa kulingana na sababu mbalimbali za matumizi hayo.

Kwa mujibu wa Mkude (2005:119) inabidi, katika mchakato huu kuvigawa vishazi hivi vyenye utendwa/utendewa katika aina nne za kauli za utendwa/utendewa ambazo ni: utendwa/utendewa unaohusisha hisia, utendwa/utendewa usiohusisha hisia, utendwa/utendewa wa kuathirika na mwisho ni utendwa/utendewa wa kupokea. Katika mgawo huu fasili ya msingi au dhima ya kila aina ya utendwa/utendewa ndiyo inayotupa mwelekeo wa kuhakiki vishazi vyenye utendwa/utendewa.

Mambo mawili yamebainika katika mchakato huu. Kwanza, si kila kauli ya utendwa ina kisawe chake cha kauli ya utendwa/utendewa. Kuna mipaka katika jambo hili. Na kwa maana hiyo, kuna vitenzi ambavyo ni: "**kuolewa**", "**kutoolewa**", "**niolewe**", "**amenioa**", "**kutolewa mahari**". Vishazi hivi havikuweza kutafutiwa visawe vyake vya kauli ya utenda kwa sababu kiima kinachokaliwa na sentensi hizo ni cha jinsia ya kike. Katika lugha hii, kitenzi "**oa**" kinabadilika na kuwa "**olewa**" katika mazingira ya kiima kukaliwa na jinsia ya kike. Kwa vile katika mahusiano haya ya kijinsiya mwanamke ni mtendewa/mtendwa, anakuwa ni mpokeaji wa matendo haya yanayohusisha mahusiano ya kijinsiya.

Jambo hili si katika lugha ya Kiswahili tu bali, katika lugha ya Rutooro ya huko Uganda matendo haya yanayohusisha jinsiya au ngono huelezwa kwa kauli ya utendwa kwa viumbe wa jinsia ya kike wakiwemo binadamu na wanyama (Kaji, 2007:264 -267). Hebu tutazame mifano hii hapa chini:

**Kuoa:** Okuswe:**ra** : kuchukua mke [kiima ni mwanaume]
Okuswe:**rwa** (+) utendwa: kuchukuliwa kama mke [kiima ni mwanamke]

**Kukutana kimwili:** okusi:hana
okucuga: [kiima ni mwanaume]
okucug**wa**: [kiima ni mwanamke]
**Kupandana** (kwa wanyama):okute:**mba** : [dume la ng'ombe]
okute:**mbwa** : (+) utendwa : [jike la ng'ombe]
Mfano mwingine ni huu:
okugobe**ka**: [mbwa dume]
okugobe**kwa** (+) utendwa: [mbwa jike]

okugo**sa** : [jogoo/kuku dume]
okugo**swa** (+) utendwa: [mtetea/kuku jike] Kaji (2007 uk 266)

**Enye mimba**
okutwe:**ka** : [kumpa mimba-kiima ni mwanaume]
Okutwe: **kwa** (+) utendwa [kupewa mimba/kiima ni mwanamke]

Jambo la pili ni kwamba, uchaguzi wa kutumia kauli ya utendwa/utendewa unachochewa na mambo mengi yakiwemo: umuhimu wa mada ya mazungumzo, kujulikana kwa mtenda wa jambo kutokana na muktadha, mbinu ya kuondoa utata ambapo kutumia kauli ya utenda kungefanya mkanganyiko katika kuelewa maana iliyokusudiwa, mbinu ya kukwepa lawama na mwisho ni kutotaka kujihusisha na mamlaka ya kimaamuzi.

Kwa kutumia nadharia zilizoelezwa hapo juu, makala hii inachambua tamthilia teule mbili za *Machozi ya Mwanamke* na *Heshima Yangu*, na katika kila tamthiliya tumepima matumizi ya utendwa/utendewa ambayo ni ya hiari na lazima. Vilevile sababu mbalimbali za matumizi ya kauli za utendwa/utendwa zimebainishwa. Na mwisho kabisa tumevigawa vishazi tendwa/tendewa katika aina nne za utendwa kama vilivyobainishwa na Mkude (2005).

### 2.1.1 Mtindo katika tamthiliya hizi

Kimtindo, tamthiliya hizi hazifanani kwani dhamira zilizoibuliwa kwenye kila tamthiliya ni tofauti kabisa. Katika tamthiliya ya *Machozi ya Mwanamke* Ngozi anaibua dhamira ya ukombozi wa akina mama wakati katika *Heshima Yangu* Muhando anaibua dhamira ya mapenzi na mvutano kati ya ukale na usasa kuhusiana na suala zima la

kuchagua mchumba wa kuolewa naye. Mwachano wa dhamira katika tamthiliya hizi umesababisha tofauti ya matumizi ya kauli za utendwa/utendewa. Katika *Machozi ya Mwanamke* Ngozi ana matumizi mengi sana ya kauli za utendwa/utendewa, na ujitokezaji huu unatokana na ukweli kwamba dhamira iliyoibuliwa inahusu ukombozi wa mwanamke ambaye anakandamizwa na mwanaume. Dhamira hii ya ukombozi dhidi ya unyanyaswaji inafanya muathiriwa wa ukandamizwaji, ambaye ni mwanamke, achomoze. Mwanamke anadai haki zake kutoka kwa mwanaume. Katika lugha ya kujikomboa kauli za utendwa/utendewa haziepukiki kutokana na kuwa mkandamizwaji, kwahiyo yeye ni mpokeaji wa matendo mbalimbali.

Vilevile muktadha wa kijamii unatofautiana katika tamthilia hizi. *Machozi ya Mwanamke* ilitungwa mara tu baada ya Umoja wa Mataifa kuutangaza mwaka 1975 kuwa ni mwaka wa akina mama kujikomboa. Kwa hiyo, mwandishi alipata msukumo wa kuiandika kazi yake akiakisi jinsi wanawake wanavyofanyiwa matendo ya kiuonevu, kiukandamizwaji, kinyanyaswaji na kidhuluma kutoka kwa wanaume.

Aina ya wahusika pia imezifanya tamthilia hizi zisifanane kwani wengi wa wahusika katika *Machozi ya Mwanamke* ni wanawake; kwa hiyo, hata mambo yanayojadiliwa kitabuni yanahusiana na lugha ya akina mama katika kuelezea masuala yao unyanyaswaji. Na vilevile katika utamaduni wa lugha hii, matendo yenye uhusiano na jinsiya au ngono huwalazimisha wanawake hawa kuyaelezea katika hali ya utendewa/utendwa huku wenzao wanaume wakiyaeleza katika utenda. Jambo hili lipo kwa yale matendo yanayofungamana na maswala ya kujamiiana.

Kipengele cha hadhira lengwa nacho kinachangia katika kutofautiana kwa tamthilia hizi. Hadira aliyoikusudia mwandishi Ngozi ni watu wa jinsia ya kike ambao wanafumbuliwa macho ili wajue haki zao mara tu ndoa zao zinapovunjika. Wanafumbuliwa macho kuwa wana haki za kugawana mali walizochuma na waume zao na pia wana haki ya kurithi watoto. Jambo hili lilikuwa gumu sana miaka ya nyuma na hata sasa katika jamii zetu za Kiafrika ambapo mfumo dume unawanyima wajane au watalaka haki ya kurithi mali. Mfumo huu unamthamini mtu wa jinsia ya kiume na kumwona kuwa ndiye mwenye haki ya kumiliki mali na watoto pale ndoa zinapovunjika. Kwa hiyo, kazi ya Ngozi ilitarajiwa iwaamshe wanawake usingizini kuhusu jinsi masuala haya ya kisheria yanavyosaidia kuwapatia haki zao walizozichuma pamoja na waume zao pale ndoa inapofikia ukomo wake.

Na kwa upande mwingine, katika tamthiliya ya *Heshima yangu* Muhando ana matumizi madogo ya kauli za utendwa/utendewa kutokana na hulka ya dhamira iliyomo katika tamthiliya hii. Suala la kupendana kati ya wawili wapendanao halishawishi matumizi ya utendwa/utendewa bali ni lugha ya kutendana (yaani kupendana). Na vilevile, kuna mgogoro wa nafsi kwa Mzee Isa ambaye hataki binti yake Rukia (ambaye ni mwanae halali) aolewe na Salum (ambaye ni mwanae haramu). Mzee Isa alifanya jambo hili kuwa siri na hakukuwa na mtu mwingine yeyote aliyeijua siri hii isipokuwa

mama wa Salum. Kwa hiyo, Mzee Isa alikuwa akiwakataza watoto hawa wasiwe na mahusiano ya kimapenzi bila kuwabainishia sababu ya msingi ya katazo hilo. Alichokuwa akikisema kilikuwa ni kisingizio tu kuwa Salum ni mtoto haramu na kwa maana hiyo, hawezi kumwoa binti yake-Rukia.

**3.0 Hitimisho na mapendekezo**

Tumeona kuwa matumizi ya kauli za kutendwa/kutendewa si jambo la hiari kwa wakati wote bali kunakuwepo na shinikizo la muktadha ambalo linamlazimisha mzungumzaji kutumia kauli ya utendwa/utendewa na si ya utenda. Jambo hili la ulazimishwaji wa kutumia kauli ya utendwa/utendewa linahusisha matendo ya kijinsiya na hata kingono ambayo hulazimisha anapotajwa mtu au mnyama wa jinsia ya kike hutumia kauli ya utendwa badala ya utenda. Vitenzi hivyo ni kama: "-olewa", "-poswa", "-chumbiwa", "-tolewa mahari" na "-tongozwa."

Kwa upande mwingine, kuna matumizi ambayo ni ya hiari ya kauli ya utendwa/utendewa ambayo yanahusisha vitenzi ambavyo havihusiani na maswala ya kujamiiana. Hapa mzungumzaji yeyote yule bila kujali jinsia yake anaweza kutumia ama kauli ya utenda au ya utendwa/utendewa ili kuwasilisha mawazo yake. Jambo la kukumbuka ni kwamba, hata katika uhiari kuna darajia za uhiari huu, kwa sababu upo utendwa/utendewa usio na mtenda, upo utendwa/utendewa wenye mtenda lakini hatajwi bayana na upo utendwa/utendewa wenye mtenda na anayetajwa bayana. Ndiyo maana tunakuwa na kauli kama: "Mtoto anaumwa", "Dirisha limevunjwa" au "Kitabu kimeazimwa na Juma"

Tunadhani kuwa kuna mapungufu katika kauli ya (Lakoff, 1975) inayodai kuwa wanawake hunyanyaswa mara mbili: kwanza kwa jinsi lugha inavyotumika kuwazungumzia wao na pili jinsi wanavyokuzwa na kufundishwa namna ya kutumia lugha. Jambo hili si kila mahali kwani tumeona wazi jinsi wanawake na wanaume katika utamaduni wa lugha ya Kiswahili wanavyoweza kutumia kauli zote mbili yaani kauli ya utenda na kauli ya utendwa/utendewa katika kuelezea mahusiano ya kijinsiya na kingono. Matendo yasiyo na uhusiano na maswala ya ngono yanamwacha mzungumzaji huru kuwasilisha mawazo yake kwa namna mbili tofauti yaani, anaweza kulisema wazo lilelile katika kauli ya utenda au utendwa/utendewa.

Yaliyoelezwa katika makala hii ni mawazo ya awali tu. Kuna haja ya kufanywa utafiti mwingine katika nyanja mbalimbali ambazo hazikushughulikiwa katika makala hii kama vile katika kazi nyingine za kifasihi ambazo hazina kabisa mwelekeo wa kijinsia ili kuona kama utendwa/utendewa unafungamana na jinsia au la. Vilevile utafiti unahitajika kufanywa katika nyanja tofauti kama vile uandishi wa kitaaluma, kisheria, uandishi wa ripoti za vikao, hatua za utafiti wa kisayansi katika maabara, maamuzi mbalimbali ya kiserikali au kiutawala, lugha za magazetini na kwingineko ili kuona ni lini lugha ya utendewa/utendewa na ya utenda hutumika au haitumiki.

## Marejeo


Crystal, D. na Davy, D (1969) *Investigating English Style*, London: Longmans.

Enkvist, N.E (1973), *Linguistic Stylistics*, The Hague & Paris: Mouton

Habwe, J. na Peter Karanja (2004), *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*, Nairobi: Phoenix Publishers

Halliday, M.A.K na Hassan R (1976), *Cohesion in English*, London: Longman.

Kabugi, C. M (1974), *Jifunze Kiswahili*, Singapore: McGraw-Hill.

Kaji, S (2007), *A Rutooro Vocabulary*, Tokyo: Tokyo University of Foreign Studies.

Khamisi, A. M (1988), "Kitenzi msingi wa muundo", *Kiswahili*, Juzuu 55/1, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Kihore, Y.M, Massamba, D. P. B na Hokororo, J.I (2001). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu*, Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Kothari, C.R (1991), *Research Methodology: Methods and Techniques*, New Delhi: Wiley Eastern Limited.

Lakoff, R (1975), *Language and Women's Place*, New York: Herper and Row

Leech, G. N na M. Short (1981), *Style in Fiction*, New York: Longman

Massamba, D. P. B, Kihore, Y.M, Msanjila, Y.P (1999), *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu*, Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili

Mkude, J (2005), *The Passive Construction in Swahili*, Tokyo University of Foreign Studies, Research Institute for Languages and Cultures of Asia and Africa (ILCAA)

Muhando, P (1974), *Heshima Yangu*, Nairobi: East African Publishing House

Ngonji, R (2006), *"Female husbands 'practice "here to stay"*, Gazeti la *Sunday Obsever*, Toleo la tarehe 02/4/ 2006, Dar es Salaam: IPP Media.

Ngozi, I (1977), *Machozi ya Mwanamke*, Dar es Salaam: Tanzania Publishing House